

## **KUWA TAYARI. ENDELEA KULINDWA NA BIMA.**

Tembelea [www.staycovered.ri.gov](http://www.staycovered.ri.gov) ili upate maelezo zaidi kuhusu usasishaji wa mpango wa Medicaid na upate usaidizi.

Tunaandika ili kukupa habari muhimu kuhusu manufaa ya bima yako ya Medicaid. Tarehe 1 Aprili, taratibu za usasishaji wa kila mwaka wa ustahiki wa kushiriki katika mpango wa Medicaid zitaanza. Taratibu za usasishaji hutusaidia kuthibitisha kwamba kila mtu anayeshiriki katika mpango wa Medicaid anaendelea kutimiza masharti.

Tulisimamisha taratibu za usasishaji wa kila mwaka ili kusaidia kurahisisha mambo wakati wa janga la afya ya umma la COVID-19 nchini. Sasa, serikali kuu inatutaka tuanze utaratibu huo tena. Tutawasiliana nawe kuhusu bima yako kati ya kipindi cha kuanzia tarehe 1 April 2023 na tarehe 31 Machi 2024. Ni muhimu tujue jinsi ya kuwasiliana nawe ili tuweze kuendelea kukupa habari wakati wa utaratibu huu.

### **UNACHOPASWA KUFANYA KWA SASA**

Hakikisha maelezo yako ya mawasiliano ni sahihi. Unaweza kufanya ifuatavyo:

1. Kwa kompyuta au simu mahiri:
  - Tembelea [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov) au pakua programu ya simu ya mkononi ya HealthyRhode na uingie katika akaunti.
  - Bofya "My Profile" (Wasifu Wangu). Kisha bofya "My Contact Information" (Maelezo Yangu ya Mawasiliano).
  - Hakikisha jina lako, anwani ya barua, nambari ya/za simu na anwani ya barua pepe. Hifadhi mabadiliko yoyote unayofanya.
  - Jisajili kupokea ujumbe wa maandishi kuhusu bima yako. Bofya "My Contact Information" kisha uchague "Sign Up for Text Messages."
2. Kwa simu:
  - Piga simu kwa nambari iliyo kwenye kadi yako ya bima ikiwa una Neighborhood Health Plan of Rhode Island, Tufts Health Plan (RITogether) au UnitedHealthcare Community Plan (UHCCP). Au, wasiliana na HealthSource RI (HSRI) kuanzia saa 8 a.m. hadi 6 p.m. siku za wiki kwa nambari 1-855-840-4774.

### **UNACHOPASWA KUFANYA ILI KULINDA MAELEZO YAKO**

Ukipigiwa simu au ukipokea barua ambayo inaonekana kuwa ni ya kimakosa, wasiliana na Kitengo cha Ulaghai (Fraud Unit) kwa nambari (401) 574-8175 au tembelea [www.omb.ri.gov/internal-audit/fraud-hotline](http://www.omb.ri.gov/internal-audit/fraud-hotline) ili uiripoti. Hakuna ada ya kusasisha maelezo yako ya mawasiliano, na Idara ya Huduma za Binadamu (DHS, Department of Human Services) na wafanyakazi wa HSRI hawapaswi kamwe kukuomba PIN au nenosiri lako. Ikiwa tunahitaji kuwasiliana nawe, unaweza kupigiwa simu kutoka DHS kwa nambari 1-855-697-4347 au HSRI. Kwa kawaida kitambulisho cha mpigaji ni HealthSource RI. Utatumiwa ujumbe wa maandishi kupitia nambari 71536.

### **UNACHOHITAJI KUJUA KUHUSU USASISHAJI WA MPANGO WAKO WA MEDICAID**

#### **Jinsi ya Kutambua Tarehe Yako ya Usasishaji**

Tambua tarehe unayotarajiwa kusasisha mpango wako wa Medicaid kwa kuingia katika akaunti yako kupitia [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov). Maelezo ya "My Renewal Information" (Maelezo Yangu ya Usasishaji) yataonyeshwa unapoingia katika akaunti.

#### **Jinsi Tutakavyokujulisha Kwamba Ni Wakati wa Kusasisha**

Utakapopokea "Recertification/Renewal Notice" (Notisi ya Usasishaji/Uthibitishaji Upya) ya manjano katika kipindi cha kati ya tarehe 1 Aprili 2023 na tarehe 31 Machi 2024, ni wakati wako wa kusasisha. Chini ya kichwa, notisi yako ya manjano itasema:

1. "The people listed below will be automatically renewed for Medicaid." (Watu waliotajwa hapa chini watasasishwa kiotomatiki kushiriki katika mpango wa Medicaid).
  - Ikiwa notisi yako inasema hivi, tafadhali angalia maelezo yaliyo kwenye notisi na utueleze ikiwa kuna mabadiliko au hitilafu zozote.

-AU-

2. "The individuals listed below are up for Medicaid renewal Some of these individuals may no longer be automatically renewed for Medicaid based on the current information in your account." (Watu waliotajwa hapa chini wanapaswa kusasisha mpango wao wa Medicaid. Baadhi ya watu hawa huenda hawawezi tena kusasishwa kiotomatiki kushiriki katika mpango wa Medicaid kulingana na maelezo ya sasa kwenye akaunti yako).
  - Notisi yako ikisema hivi, utapokea hivi karibuni notisi ya "Additional Documentation Required". Unapoipokea, tafadhali tafuta hati zinazohitajika na uziwasilishe kwetu kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa kwenye notisi.
  - Kadiri tarehe yako ya mwisho inapokaribia, tutakutumia kikumbusho cha kuwasilisha maelezo yako ikiwa hatujayapokea.

### **Unachohitaji Kujua Kuhusu Hali Maalum**

Utaratibu wa usasishaji wa mpango wa Medicaid utakuwa tofauti kwa watu wengine walio na hali maalum zinazoathiri ustahiki wao. Ikiwa tutajua kwamba wewe ni mmoja wao, hutapokea notisi ya manjano. Utapokea Notisi ya kijani ya "Special Circumstance" (Hali Maalum) inayokueleza unachopaswa kufanya.

Ikiwa umejiondoa katika huduma ya kupokea hati kupitia barua pepe, unaweza kusoma notisi zako zote kwenye akaunti yako ya mtandaoni katika [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov).

### **JINSI YA KUWASILISHA HATI ZINAZOHITAJIKA**

Unaweza kuwasilisha hati fulani zinazohitajika kwa kuingia kwenye akaunti yako katika [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov) au kwa kutumia programu ya HealthyRhode.

Ili kuwasilisha fomu yako uliyotia saini ya usasishaji wa mpango wa Medicaid, pamoja na hati zingine zinazohitajika, unaweza:

- Kutembelea RI DHS Scan Center iliyoko 1 Reservoir Ave. katika jiji la Providence kati ya saa 8:30 a.m. na 4 p.m., Jumatatu hadi Ijumaa (isipokuwa siku za likizo). Kuja na hati zako ili mfanyakazi wetu aweze kuzichanganua na kuzihifadhi kwenye mfumo wetu.
- Kutuma hati kwa barua (tafadhali tuma nakala pekee na ubaki na hati halisi) kwa P.O. Box 8709, Cranston, Rhode Island 02920-8787

Baada ya kufaulu kuwasilisha maelezo yako, tutakutumia notisi ya shukrani. Hiyo inamaanisha kwamba tumepokea maelezo yako na tunayakagua.

### **JINSI TUTAKAVYOKUJULISHA KUHUSU HALI YA BIMA YAKO**

Baada ya kushughulikia ombi lako la usasishaji, utapokea "Benefit Decision Notice" (Notisi ya Uamuzi wa Manufaa). Notisi hii itakufahamisha ikiwa bima yako ya Medicaid imeidhinishwa au imekataliwa. Ukinyimwa bima, Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako itakufahamisha kuhusu chaguo nyingine za kuendelea kupokea huduma ya bima.

- Ikiwa unastahiki kupokea bima ya HealthSource RI inayofadhiliwa na Jimbo kwa miezi miwili, Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako itajumuisha maelezo haya.
- Ikiwa hukubali uamuzi wetu kuhusu manufaa yako, unaweza kukata rufaa kwa kufuata utaratibu ulioelezwa kwenye Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako.

Tembelea [www.staycovered.ri.gov](http://www.staycovered.ri.gov) ili upate maelezo zaidi kuhusu usasishaji wa mpango wa Medicaid na jinsi ya kupata usaidizi.